JOURNAL OF INDIGENOUS LANGUAGES
Jozac Publishers
Vol. 2, No. 1, 2024
**Website:** http://journals.jozacpublishers.com/jil
*Type of the Paper: (Article Paper)*

# Uhusika katika lugha ya Kiswahili

**Igunza Onzere[1*], Faraja Kristomus Lugome[2], Mendong Margaret[3]**
[1*]Advanced School of Translators and Interpreters (ASTI), University of Buea, Cameroon. shaddy.igunza@gmail.com, https://orcid.org/0009-0005-7250-7403
[2]Department of Foreign Languages and Linguistics, University of Dar es Salaam, Tanzania. farajalugome@gmail.com
[3]Department of Sociology and Anthropology, University of Buea, Cameroon. mendongcube@yahoo.com, https://orcid.org/0000-0003-1845-1689

Correspondence: shaddy.igunza@gmail.com

**Received:** 03 July 2024; **Accepted:** 27 August 2024; **Published:** 15 October 2024

**Abstract:** This study explores Case Semantics in linguistics, specifically in the Swahili language. The concept of Case Semantics deals with how noun phrases function in a sentence and its relation to the verb. Case Semantics is integral in everyday language use and many at times language users encounter it unconsciously. The concept of case semantics coincides with many areas of linguistics such as; Semantics, syntax, phonology, and even morphology. The main focus of this study are; to explicit the concept of case semantics in Kiswahili according to different scholars and linguists with our inputs factored in, to highlight the types of case semantics that exist in the Kiswahili language, and finally to explain their importance and recommendations. The main data used is secondary data that was collected from library and online articles. Questionnaires and interviews were also used to obtain sufficient data to justify the outcome of this study. The types of case semantics that were identified are the; agent, patient, instrument, result, force, goal, cause, location, range, and material case semantics. This study outcome proves case semantics as an important concept in learning language skills in a way that; it enables the language user to recognize the importance of the case semantics in Swahili language, to know its correct use, and thus avoid its incorrect use. In addition, the identification of the case helps the scholar and language researcher to know other language concepts that are close or related to case semantics such as clauses and phrases.

**Keywords:** Case semantics, Clause, Linguistics, Phrase, Swahili language

**Ikisiri:** Utafiti huu unaangazia Uhusika katika lugha ya Kiswahili. Dhana ya uhusika ni dhana inayopambanua majukumu ya nomino katika sentensi na uhusiano wake na vitenzi. Watumizi wa lugha wanatagusana na kutumia uhusika kwenye sehemu kubwa ya matamshi na maandishi ya lugha kila siku na wakati bila hata kutambua. Dhana ya uhusika inajipenyeza kwenye mawanda mengi ya isimu kama vile; Semantiki, sintaksia, fonolojia na hata mofolojia. Utafiti huu unaazimia kufafanua maana ya dhana ya uhusika kulingana na wanaisimu mbalimbali mchango wetu ukiwemo, kuweka wazi aina za uhusika ambao unapatikana katika lugha ya Kiswahili na mwisho kabisa kueleza umuhimu wa uhusika katika lugha ya Kiswahili pamoja na mapendekezo. Data msingi iliyotumiwa kwenye utafiti huu ni data ya sekondari ambayo ilitafitiwa maktabani na kwenye makala ya mitandaoni. Hojaji na dodosa pia zilitumiwa ili kupata data ya kutosheleza kutetea matokeo ya utafiti huu. Aina ya uhusika ambao ulitambuliwa na kushughulikiwa ni pamoja na uhusika wa mtenda, mtendwa, mtendewa, ala, tokeo, nguvu, lengo, chanzo, mahali, mapito na


OPEN ACCESS

malighafi. Matokeo yanabaini kuwa uhusika una umuhimu mkubwa sana kwenye stadi ya isimu kama vile; Kumwezesha mtumizi wa lugha kutambua uhusika ulioko kwenye lugha ya Kiswahili, kujua matumizi yake sahihi na hivyo kuepuka kuutumia visivyo. Zaidi ya haya yote, utambuzi wa uhusika humsaidia msomi na mtafiti wa lugha kujua istilahi na dhana zingine za lugha ambazo zinaambatana ama kukaribiana na uhusika kama vile virai na vishazi.

**Istilahi:** Isimu, Kiswahili, Uhusika, Virai, Vishazi

## 1. Utangulizi

Dhana ya uhusika ni dhana ya kisarufi ambayo hutumiwa kuonyesha dhima ya maneno katika tungo, semi au sentensi. Dhana hii ni muhimu sana katika uchambuzi wa tungo maana hutumiwa kuwasilisha ujumbe wa kisemantiki haswa muundo wake wa ndani (Fillmore, 1968). Dhana ya uhusika ilikuwa na misingi yake ndani ya nadharia ya umuundo iliyoibuliwa nchini Czechoslovakia na waasisi kama vile; Roman Jacobson, Trubetzkoy Jan Mukarovsky na Boris Tomaserky. Wasomi hawa walijiita wana Prague katika kuendeleza mawazo yao ya kitaaluma na kilugha. Hata hivyo, waasisi hawa wa umuundo walitumia mawazo ya Ferdinand de Saussure ambaye alikuwa na mtazamo tofauti wa dhana mbalimbali za kiisimu. Hii mitazamo yake, aliwafundisha wanafunzi wake kupitia mihadhara mbalimbali aliyokuwa nayo nao; Culler (1975:4-5). Wanafunzi wake baadaye walichapisha mawazo ya mwalimu wao wakiongozwa na Charles Bally kwenye kitabu "A course in General Linguistics" mwaka wa 1916.

De Ssausure aliibua dhana ya 'Langage' ambayo ni lugha ijulikanayo na kutumiwa na jamii, 'Langue' ambayo ni sheria na kanuni za lugha pamoja na 'parole' ambayo ni matumizi ya lugha katika mazungumzo na maandishi. Hivyo basi, msimamo wa umuundo kulingana na De Ssausure ni kuwa; lugha inafaa kuchukuliwa kama mfumo wa ishara zinazohusiana, kuwa kuna kiashiria na kiashiriwa kwenye mfumo wa matumizi ya lugha. Mfano, tukizungumzia meza; nomino meza ni kiashiria cha kifaa-meza ambacho hutumiwa kuandikiwa, kusomewa au kulia chakula. Hivyo basi, kuna uhusika au uhusiano baina ya kiashiria na kiashiriwa. Alielezea zaidi kuwa maana ya ishara hueleweka kutokana na uhusiano unaotokana na viwango mbalimbali kama ishara za kimlalo na kiwima.

Nadharia ya X-ba nayo iliipa misingi nadharia ya umuundo aliyokuja kuijenga na kuiendeleza Charles Fillmore kwenye dhana ya uhusika. Nadharia ya X-ba iliasisiwa na Jackendoff (1977) na ikaja baadaye kuendelezwa na waasisi wengine. Nadharia hii ya x-ba ilitokea ili kuziba mapungufu ya nadharia ya Sarufi miundo virai ambayo ilikuwa na sheria nyingi zilizohusisha kategoria mbalimbali katika uwakilishi wa miundo ya sentensi. Chomsky (1981) alikuja kuunda nadharia ya sarufi bia ambayo inabainisha sifa bia za sarufi, na sifa hizi zinahusisha lugha zote za ulimwengu.

Nadharia ya X-ba inawakilishwa na kategoria X ambazo zinawakilisha kategoria zote za kileksika yani; Nomino, Vitenzi, Vivumishi, Vihusishi na Vielezi. Kutokana na nadharia hii, Kirai ndicho kiambajengo muhimu katika uchanganuzi. Nadharia hii awali ilitumika katika kuonyesha miundo ya virai pekee vilivyoundwa kutokana na kategoria za kisarufi kama vile Nomino, Vitenzi, Vivumishi, Vielezi na Vihusishi lakini baadaye wanaisimu kama vile Charles Fillmore wakaja kuongeza kategoria za kiuamilifu kama vile vibainishi, Kiima, yambwa, vijalizi na hata viambishi awali vya mnyambuliko katika vitenzi ili kuleta usawazisho wa kimuundo.

Kwa wepesi, tunaweza tukafafanua uhusika kuwa ni namna maneno yanavyotekeleza majukumu yake katika sentensi. Majukumu ya maneno katika sentensi huwa na utegemezi mkubwa wa kitenzi kikuu katika sentensi. Maneno haya yanaweza kutekeleza majukumu mengi kwenye sentensi; mfano, nomino inaweza kutaja jina, kitenzi kitaonyesha kinachofanywa au kutendeka kwenye sentensi, kivumishi kitatoa sifa au kuvumisha nomino na kiwakilishi, kiwakilishi kitafanya jukumu la kuwepo kwa niaba ya Nomino.

Hata hivyo, Charles Fillmore kwa upande wake alifafanua na kuboresha uhusika muda baada ya muda na kusema kuwa; uhusika ni majukumu ambayo yanatekelezwa na nomino katika sentensi. Huu ndio ufafanuzi ambao utatuongoza na kutuelekeza katika kufasiri uhusika katika Kiswahili kwenye utafiti wetu.

## 2. Nadharia ya utafiti

Utafiti huu ulijikita kwenye nadharia ya umuundo ya Ferdinand De Saussure (1916). Misingi ya nadharia hii ilikuwa kwenye stadi ya semiotiki (stadi ya ishara). Nadharia hii inasisitiza kuwa tunafaa kuiangalia lugha kama mfumo wa ishara zinazohusiana. Anaendelea kueleza kuwa lugha inajengwa na kiashiria na kiashiriwa. Kiashiria ikiwa ni lugha na kiashiriwa kikiwa ni kile ambacho kinarejelewa ama kinalengwa. Mfano; neno simu ni kiashiria maana linawakilisha kifaa halisi kiitwacho simu ambacho kinatumiwa katika mawasiliano.

De Ssausure anaendelea kuelezea kuwa lugha huwa inaelezeka kutokana na uhusiano ambao aidha unaweza kuwa uhusiano wa Kiwima (kiparadigma) na uhusiano wa kimlalo (kisintagma). Uhusiano wa kiwima ni uhusiano ambao ni wa kiuteuzi na maneno kubadilishana, nao uhusiano wa kimlalo ni uhusiano wa kiuhusiano na kimuingiliano ili kuunda tungo sahihi. Uchunguzi wa tungo za Kiswahili hujikita sana sana kwenye uhusiano wa kimlalo japo wa kiwima kwa kiwango kidogo tu.

Nadharia ya umuundo inahusiana na utafiti huu kwa kiwango kikubwa sana. Mwanzo, utafiti wetu unaangazia uhusika, dhima na umuhimu wa uhusika katika sentensi za Kiswahili. Hapa bila shaka, tungo za Kiswahili na miundo ya tungo hizi imeangaziwa ndiyo inachunguzwa kwa kigezo cha uhusika. Uhusika kwa hakika ni uhusiano wa nomino na istilahi zingine za lugha kwenye sentensi pamoja na majukumu ya nomino hizi bila kusahau umuhimu wa uhusiano huu. Hivyo basi, umuundo ni nadharia muhimu ya kuegemeza utafiti huu maana utafiti unajikita kwa miundo ya tungo za Kiswahili kwa mkabala wa majukumu ya nomino.

Utafiti huu ulifanywa pia kwa misingi ya nadharia ya semantiki tambuzi. Sematiki tambuzi ni mwelekeo wa kinadharia ambao unajikita kwa masuala ya akili na uhusiano wake katika tajriba jumuishi pamoja na utamaduni. Taaluma ya semantiki tambuzi ilianza kushughulikiwa miaka ya 1970 huku ikijaribu kupinga na kutoa mwelekeo wa nadharia ya mtazamo wa ulimwengu wa malengo (objectivist worldview theory) uliokuwa na mwonekano wa kimapendeleo sana.

Mihimili ya nadharia hii ya semantiki tambuzi inadai kuwa maana ni dhana, kumaanisha kuwa maana haiko kwenye maneno yenyewe ila kwa kitajwa chenyewe ambacho kiko akilini(utambuzi) mwa mzungumzaji na mzungumziwa. Maana ni mifumo ya picha inayoundwa akilini maneno yanapotajwa na kuzungumzwa. Uwakilishi wa maana akilini ni kama seti ya vitabu vinavyotoa taarifa kuhusu mambo mengi (representation of meaning is encyclopaedic) na muundo wa maana huhusisha utambuzi. Wataalamu wanaotajika kuendeleza nadharia hii ni kama vile (Talmy, 1981, 1985, 2000; Lakoff, 1980, 1987).

Nadharia ya semantiki tambuzi ina umuhimu sana kwa utafiti wetu maana utafiti wetu unajaribu kuangalia uhusika katika sentensi za Kiswahili. Uhusika unajikita kwenye utathmini wa majukumu ya nomino katika sentensi na majukumu haya hutathminiwa akilini, kumaanisha kuwa, utambuzi lazima ufanywe kutokana na tajriba ya akili na ufahamu wa kijumla. Kufanikisha haya, nadharia ya semantiki tambuzi lazima itiliwe mkazo na kuzingatiwa.

## 3. Mbinu za utafiti

Data iliyotumiwa kuafikia matokeo ya utafiti huu ilipatikana kwa utafiti wa data sekondari. Hapa, vitabu vingi vya kuaminika, waandishi wenye tajriba kwenye uwanja wa isimu na mahsusi semantiki walizingatiwa. Makala vilevile yaliyo maarufu na yenye kubeba data muhimu ya kuzingatiwa kwenye utafiti huu ilitiliwa maanani.

Mbinu ya hojaji za mitandaoni kupata maoni ya wataalamu kwenye uwanja huu wa isimu na semantiki walihojiwa ili kutoa michango yao kuhusu uhusika, aina ya uhusika na vilevile umuhimu wa uhusika kwa jumla kwenye lugha ya Kiswahili. Wataalamu 62 wa Kiswahili wakiwemo wanafunzi, walimu na wahadhiri waliobomea kwenye masuala ya isimu na semantiki ndio walihojiwa kutumia hojaji.

**Jedwali la 1**: Watafitiwa

| Kundi la watafitiwa | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|
| Wahadhiri wa Isimu | 12 | 10 | 22 |
| Wanafunzi wa chuo wa isimu | 15 | 15 | 30 |
| Walimu wa lugha wa sekondari | 5 | 5 | 10 |
| | | | 62 |

## 4. Matokeo ya utafiti

Baada ya utafiti wa kina kutoka kwa wataalamu wengi ambao wamenukuliwa ndani ya makala haya na kuwawekea marejeleo hapa chini, kuhusu mtazamo wao kwenye suala la uhusika, aina zifuatazo za uhusika zilizitokeza kwenye lugha ya Kiswahili;

### 5.1. Uhusika Mtenda

Mtenda ni mtu au kitu kinachotekeleza kitendo kwenye sentensi. Kwa kingereza ni *agent*. Huu ni uhusika kwenye sentensi ambao nomino ina jukumu la kutekeleza kitendo katika sentensi. Kwa mujibu wa Fillmore (1968), nomino au kiwakilishi kinapotumika kama kiima cha kitenzi, hutambulishwa kuwa uhusika wenye kutekeleza jukumu la kutenda. Huu ni uhusika ambao hujibu swali la; ni nani aliyetenda kitendo fulani? Hivyo basi, uhusika huu huhusisha vitu vyenye uhai kama vile binadamu, wanyama na hata wadudu ambavyo husisimua utendaji wa tendo. Kando na kuhusisha viumbe hai pekee, vilevile roboti inaweza kujumuishwa kwenye uhusika mtenda kwani ni vitu vyenye uwezo wa kutenda kitendo ambacho kiumbe hai chaweza kutenda. Mfano kwenye sentensi;

i) **Baba** anampiga mtoto
ii) Wimbo unaimbwa na **msichana**

Kwenye sentensi (i), baba ndio mtenda, anafanya kitendo cha kupiga. Sentensi ya (ii) nayo msichana ni uhusika wa mtenda maana ndiye anatekeleza jukumu la kuimba.

### 5.2. Uhusika mtendwa/kitendwa

Uhusika huu hurejelea nomino inayoathiriwa moja kwa moja na kitendo au matukio ya mtendaji kwenye sentensi, Fillmore (1968). Kwa Kingereza ni *patient*. Mtendwa anaweza kuwa hai au hata asiwe hai. Mfano;

i) **Mtoto** amebebwa
ii) **Chakula** kimepikwa

Kwenye sentensi hizi; (i) Mtoto ni mtendwa maana anapata athari za kitendo cha kubebwa. Kwenye sentensi (ii) Chakula ndio kitendwa maana kinapitia athari za kupikwa (kutayarishwa kuwa tayari kuliwa), chakula si nomino hai.

Wataalamu wengi wamedadavua uhusika wa mtendwa kama vile Talmy (2000) aliyeuangalia uhusika huu kwa mwelekeo wa Kiutambuzi. Yeye anasema kuwa majukumu ya Kisemantiki kama vile mtendwa yanatokana na michakato yetu ya utambuzi wa ulimwengu. Hivi ni kusema kuwa, tunapotumia lugha huwa tunategemea mifumo ya utambuzi ili kuelewa uhusiano uliopo kati ya vitu na matukio yenyewe. Mfano, kwenye sentensi (ii) tukiambiwa kuwa chakula kimepikwa, utambuzi wetu wa kiakili utaturejesha kwenye shughuli nzima ya utayarishaji chakula na kujua hatua ambazo chakula kilipitia wakati kikipikwa.

Fillmore(1968) anasema kuwa, uhusika wa mtendwa huashiria hisia za tendo. Uhusiano uliopo hapa ni wa moja kwa moja kati ya mtenda, pigo na mtendwa. Kutokana na mahusiano haya, suala la mfuatano wa maneno katika sentensi hutumika ndipo kubainisha tofauti kati ya jukumu mtenda na jukumu mtendwa au mtendewa.

Suala la mfuatano wa vitendo wa maneno katika sentensi ni muhimu kwani hutambulisha taipolojia ya kisintaksia ya lugha. Kittila, Vista na Ylikoski (2011) wanasema kuwa, mfuatano wa maneno katika sentensi iliyo na uhusika mtendwa ni kama ifuatavyo: iwapo sentensi ipo katika hali ya kauli ya kutenda, kiima hutanguliza huku kitenzi kikuu kikifuata na baadaye mpokezi wa pigo. Iwapo sentensi ipo katika hali ya kauli ya kutendwa, mpokezi wa pigo huitanguliza kisha hufuatwa na pigo lenyewe na baadaye mtendaji wa tendo. Hoja hii ndiyo itakayomwongoza mtafiti katika suala zima la kubainisha uhusika wa mtendwa. Aghalabu, maumbo ya uhusika mtendwa hutawaliwa na viwakilishi nafsi vya pili na tatu umoja na wingi. Viwakilishi nafsi huru hivi huwekwa katika nomino ambazo huhusishwa na kundi la binadamu pekee. Katika virai nomino ambavyo havihusishwi na kundi la binadamu, viwakilishi faafu kisintaksia huchukua nafasi ya virai nomino hivyo na kuwa umbo la uhusika

### 5.3. Uhusika mtendewa/kitendewa

Uhusika mtendewa/kitendewa ni uhusika ambao nomino huathirika na athari za kitendo, ila si athari ya moja kwa moja (Fillmore, 1968). Kwa Kingereza ni *experiencer.* Ni sahihi kusema kuwa uhusika wa mtendewa ni uhusika ambao nomino inatendewa kitendo kwa ajili yake. Hivi ni kusema kwamba, nomino (mtendewa) ilifaa kutenda kitendo fulani ila ikatendewa na nomino nyingine kwa niaba ya nomino hiyo.

Mtendewa na mtendwa wana usawa na ukaribu sana ila tofauti ni kuwa mtendwa anapata athari ya tendo moja kwa moja, ila mtendewa anapata athari ya tendo kupitia mtenda (Dowty, 1991). Wote mtendwa na mtendewa wanaweza kuwa viumbe hai au hata wasiwe viumbe hai, ila wana uwezo wa kupokea athari ya kitendo.

Mifano ya mtendewa/kitendewa kwenye sentensi ni kama vile;

i) *Maria alimlimia **Sofia** shamba*
ii) ***Nyanya** alisomewa barua na jirani*

Kwenye sentensi hii (i) Sofia ndiye alistahili kulima shamba, ila kulima huku kukafanywa na Maria kwa niaba ya Sofia. Hivyo basi, sofia anakuwa mtendewa. Sawasawa na sentensi ya (ii) ambayo nyanya alifaa kusoma barua ila ikasomewa kwa niaba yake na jirani. Hivyo, nyanya ni mtendewa.

### 5.4. Uhusika ala

Uhusika huu vilevile unatambulika kama uhusika kifaa. Uhusika wa ala huashiria chombo ambacho hutumika kutenda tendo, Fillmore (1968). Hata hivyo, uhusika ala ukishatenda kitendo, huwa hauathiriwi tena. Kwa kingereza uhusika huu hujulikana kama *instrument.*

Mifano kwenye sentensi;

i) *Mgeni alikunywa uji kwa **kijiko**.*
ii) *Waziri alisafiri kwa **ndege***

Kwenye sentensi (i), kijiko ndio ala maana kimesaidia kitendo cha kunywa uji kutendeka. Hata hivyo, baada ya kitendo cha unywaji uji, kijiko hakihusiki tena, au hakiathiriwi tena.Kwenye sentensi (ii), ndege ni ala maana inaonyesha kifaa kilichotumiwa kwenye shughuli ya usafiri.

Mahusiano kati ya kiima na kiarifu katika sentensi hubainisha kifaa kilichotumika kutendea tendo hilo. Kifaa hicho ni uhusika ala. Ala si mojawapo ya nomino za kundi la kwanza na la pili la kimofolojia, hivyo basi, aina nyingine ya viwakilishi isipokuwa vya nafsi ina nafasi ya kuwa umbo la uhusika kwenye sentensi. Uteuzi wa kiwakilishi faafu kuchukua nafasi ya kirai nomino chenye uhusika ala ni lazima utilie maanani usahihi wa sentensi kimuundo na kisarufi.

Nguzo kuu katika kubaini uhusika ala ni kujibu swali; ni kifaa gani kilichotekeleza tukio fulani? Ufahamu huu hurahisisha kabisa uelewaji wake kuhusu suala linalogusiwa na kuleta fasili moja ya maana kisemantiki katika kichwa cha makala teule.

### 5.5. Uhusika Tokeo

Uhusika wa matokeo ni kile ambacho kinatokana na kitendo cha malighafi ya kitendo. Kwa Kingereza ni *result*. Kwenye uhusika huu, mtu hujiuliza; baada ya mchakato wote wa matukio kwenye sentensi, nini mwisho wake? Ama matarajio ni gani baada ya mchakato wote kwenye sentensi?

Mifano kwenye sentensi;

i) *Seremala aliunda **mlango** kutoka kwa mbao.*
ii) ***Kufaulu** kwake kulichangiwa na bidii*

Mlango hapa kwenye sentensi (i) mlango ni uhusika wa tokeo maana mlango huo unatoka kwa mbao. Au kiufupi tunaweza kusema, mlango ni tokeo la mbao. Kufaulu ni tokeo la bidii kwenye sentensi ya (ii).

Dowty (1991) anadadavua zaidi uhusika huu kwa kusema kuwa tokeo linaweza kuwa chanya au hasi. Vilevile tokeo linaweza kuwa linaloathiriwa moja kwa moja na mchakato mzima wa sentensi, au liwe lile tokeo ambalo haliathiriwi moja kwa moja na mchakato. Linaweza kuwa tokea thabiti au ambalo linaonekana, ama liwe tokeo ambalo linakisiwa tu litatokea bila kutajwa moja kwa moja na sentensi. Vilevile anasema kuwa, tokeo linaweza kuwa moja tu, au iwe misururu ya matokeo kadhaa kwenye mchakato wa matukio ya sentensi.

### 5.6. Uhusika nguvu

Uhusika huu ni uhusika ambao unafanya kitu au unatenda kwenye sentensi. Vilevile linaweza kuelezwa kama ni kisababishi kwenye sentensi. Fillmore (1968) kwenye maelezo zaidi alisema kuwa nguvu inawakilisha sababu ya 'nje' kwenye matukio ambayo kwa hakika haina hiari ya yale ambayo yanatukia kwake.

Mfano;

*i)* ***Jua*** *lilinyausha mimea*

*ii)* *Wanyama waliuawa kwa* ***radi***

Kwenye sentensi hii(i), kisababishi cha mimea kunyauka ni jua, sentensi ya (ii) nayo radi inakuwa ndio nguvu. Hivyo, jua na radi ndio vinakuwa ni uhusika wa nguvu kwenye sentensi hizi.

Nguvu inaweza kuwa kitu chenye uhai au hata kitu kisicho na uhai ila kinaishia kusababishia kitu kingine athari kutumia nguvu zake kilicho nazo, Langacker (1987). Kwenye mfano wetu (i), Jua lina nguvu ya kunyausha kwenye hii sentensi. Sentensi ya pili nayo, radi ina nguvu za kusababisha mauaji

Tofauti kati ya uhusika nguvu na mtenda ni kuwa, mara nyingi huwa kiumbe chenye uhai, mtenda anaweza kutenda kwa hiari au wakati mwingine kusiwe na hiari. Nguvu kwa upande wake huwa kitu kisicho na uhai, hufanya majukumu au mambo yake bila kusudi wala nia na hakuna hiari ya kupokea na kutopokea athari za nguvu.

### 5.7. Uhusika lengo

Uhusika lengo ni uhusika ambao unaonyesha kitu kinacholengwa kwenye sentensi. Aidha, ni makadirio, matamanio au maazimio yanayofaa kuafikiwa. Kwa kingereza huitwa *goal*. Kwenye uhusika huu, hatima ya sentensi au ya mtendaji kwenye sentensi ndio huchanganuliwa kama lengo la mtenda au lengo la sentensi nzima. Mfano kwenye sentensi;

*i)* *Mchungaji anaelekea* ***kanisani***

*ii)* *Wanafunzi wanaazimia kupata* ***matokeo mazuri***

Kwenye sentensi hizi, lengo la mchungaji ni kuingia kanisani, na hivyo kanisani itakuwa ndio lengo kwenye sentensi hii maana ndio matarajio na hatima ya mchungaji. Sentensi ya pili ya pili nayo, Lengo na maazimio ya wanafunzi ni kupata matokeo mazuri

Mel'cuk (1998) aliendeleza utafiti huu kutoka kwa mwalizishi Fillmore (1968) kwa kusema kuwa, lengo linaweza kuwa lengo kuu au lengo mahsusi na hata lengo dogo. Vilevile malengo haya yanaweza kuwa malengo ya muda mfupi au hata yakawa ya muda mrefu, mradi tu yawe bayana kwenye sentensi.

### 5.8. Uhusika chanzo

Uhusika huu pia hujulikana kama uhusika wa Kisababishi. Hujaribu kuonyesha mahali ambapo kitu fulani au tuseme tendo fulani lilikoanza kutokea, Fillmore (1968). Kwa Kingereza ni *Cause.* Mfano kwenye sentensi;

*i)* *Ugonjwa wa malaria hutokana na* ***mbu***

*ii)* ***Ufisadi*** *huleta umaskini*

Kwenye sentensi (i), sababu ya kuwa na ugonjwa wa malaria ni kuumwa na mbu. Hatima ya malaria haiwezi kuwepo bila kitendo cha mtu kuumwa na mbu kutokea. Sentensi (ii) Ufisadi ndio chanzo cha umaskini kulingana na sentensi hii.

Hivyo basi, uhusika wa chanzo ni muhimu maana hutupa mwelekeo wa leo au tamati inayosababisha jambo fulani kutukia kwenye sentensi. Talmy (2000) kwenye utafiti wake uliohusisha kuoanisha Uhusika na semantiki tambuzi aliendelea kueleza kuwa, dhana ya asili ya kitu au tukio hutegemea sana, au hutokana na uzoefu-ulimwengu wetu. Hii ni pamoja na utambuzi wa masuala na matukio yanayopatikana kwenye mazingira pamoja na uelewa wetu kwa jumla.

### 5.9. Uhusika mahali

Uhusika huu huwakilisha eneo la tukio, kitu au hata hali kwa kuonyesha sehemu ambayo kitendo kilitukia kwenye sentensi. Kwa kingereza huitwa *location*.

Uhusika huu vilevile unaweza kuonyesha mazoea ya tendo kutendeka mahali fulani (Langacker, 1987). Mifano ya uhusika wa mahali kwenye sentensi ni kama vile;

i) *Maombi hufanywa **kanisani***
ii) *Alinitembelea **nyumbani***

Kwenye sentensi hii (i) mahali ambapo maombi hufanywa ni kanisani na ndio uhusika wa mahali ambapo ibada za wakristo hufanyika. Vilevile kwenye sentensi (ii) mahali ambapo mtenda alimtembelea mtendewa ni nyumbani. Hivyo basi, nyumbani ni uhusika wa mahali.

Kwenye uhusika wa mahali, mara nyingi kiambishi tamati-ni cha kuonyesha ndani huwekwa kwenye nomino ya mahali, kuonyesha kuwa ni ndani ya. Vilevile vihusishi kama vile 'katika', na 'kwenye' hutumiwa kuonyesha mahali panaporejelewa kwenye sentensi. Mfano kwenye sentensi (iii) ifuatayo';

iii) ***Katika pango** hilo ndipo alipoonekana chatu*

### 5.10. Uhusika mapito

Uhusika mapito kwa kingereza huitwa *range*. Uhusika huu huonyesha yaliyotokea katikati ya chanzo na lengo.

Mfano kwenye sentensi;

i) *Rais alisafiri kwenda Eldoret kupitia **Kisumu**.*
ii) *Alice alimtembelea **Juma** wakati alikuwa akielekea nyumbani*

Uhusika wa mapito humwelekeza mtendaji kufikia hatima. Mapito huzingatiwa kwenye sentensi maana kupitia kwa mapitio ndio mtendaji hujipata tamati au kwenye lengo. Kwenye sentensi (i), kufika kwa rais Kisumu kulitegemea mapitio yake Kisumu kabla ya kufika Eldoret. Sentensi (ii), kabla ya Alice kufika nyumbani, alipitia kwa Juma.

### 5.11. Uhusika malighafi

Kwenye uhusika huu, vifaa vinavyotumiwa kutekeleza vitendo kwenye sentensi ndivyo huzingatiwa. Uhusika huu ni muhimu maana hutusaidia kuelewa tokeo linatoka wapi, au tokeo linatoka "kwa nini". Uhusika huu kwa Kingereza ni *materials.* Mfano;

i) *Mwashi alijenga nyumba kwa **mawe**.*
ii) *Ugonjwa wake uliponywa kwa **dawa***

Mbao zinakuwa malighafi kwenye sentensi (i) maana ndio vifaa vinavyosaidia kufanikiwa kutendeka kwa tendo la ujenzi. Malighafi pia inaweza kuchukuliwa kama msaidizi au kisaidizi cha mtenda ili kumsaidia kufanikisha tendo lake, Langacker (1987). Mfano kwenye sentensi (ii), Kupona kwa mgonjwa kulisaidiwa au kuliwezeshwa na dawa ambayo ilisaidia kuwepo na kupona. Hivyo, dawa inakuwa malighafi.

## 5. Umuhimu wa uhusika katika lugha ya Kiswahili

Stadi ya uhusika ni ya kufaa sana maana inasaidia wanalugha kujua matumizi sahihi ya uhusika kwenye sentensi na hivyo lugha kuendelezwa inavyofaa na inavyostahili na hivyo kuepuka makosa mengi ya kimatumizi ambayo yangejitokeza kwa kukosa kujua mwao wa matumizi ya uhusika.

Uhusika unasaidia kufafanua maana ya sentensi kwa kutengeneza uhusiano wazi kati ya maneno na majukumu yanayojitokeza katika kitendo au tukio linaloelezewa kwenye sentensi.

Uhusika unachangia sana katika kuelewa mifumo ya sarufi ya lugha mbalimbali. Kwa kuchanganua jinsi lugha zinavyotumia uhusika kuashiria majukumu ya maana, wataalamu wa isimu wanaweza kupata ufahamu bora wa jinsi sarufi inavyofanya kazi na jinsi lugha zinavyotengeneza maana.

Uhusika unatumika sana katika utafiti wa lugha, haswa katika nyanja za semantiki ya lugha, isimu-linganishi, na isimu-tambuzi. Kwa kuchanganua uhusika katika lugha tofauti, watafiti wanaweza kulinganisha jinsi lugha zinavyofikiria na kuelezea ulimwengu unaowazunguka.

## 6. Hitimisho

Kutokana na utafiti huu, ni bayana kuwa, stadi ya uhusika ni sehemu kubwa na muhimu ya isimu ya Kiswahili inayofaa kutiliwa maanani maana inatekeleza majukumu muhimu katika sentensi na lugha kwa jumla. Kupitia upambanuzi uliofanywa na wataalamu wengi, nomino kama kategoria ya kileksika na majukumu yake kwenye sentensi sasa ni suala linaloeleweka vizuri.

Hata hivyo, stadi hii ina upungufu wake maana inajikita kwenye ufaafu wa sentensi pekee na kuacha vipengele na istilahi zingine muhimu za lugha kama vile uchukuliaji kwenye pragmantiki. Vilevile, bado kuna utata kuhusiana na uhusika, lugha tofauti zina njia tofauti za kuwasilisha uhusika wake na hivyo kuchukulia kijumla kuwa lugha zote za ulimwengu huwa na mfumo mmoja wa uhusika, hili si kweli.

## 7. Mapendekezo

Utafiti huu haukufanikiwa kuguzia mawanda yote yanayohusiana na uhusika kwa sababu ya muda na rasilimali. Kupitia utafiti huu itakuwa vizuri sana kama utafiti zaidi utafanywa kuhakiki kama uhusika huuhuu unavyojitokeza kwenye sentensi ndivyo unavyojitokeza kwenye mawanda mengine ya isimu.

Vilevile, itakuwa bora kabisa kama utafiti zaidi utafanywa ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza baina ya uhusika, chagizo na shamirisho.

## Marejeleo


1. Bernard, C. (1989). *Language universals and linguistic typology*. University of Chicago Press.
2. Chomsky, N. (1980). *Rules and representations*. Blackwell.
3. De Saussure, F. (1916). *Course in general linguistics*. McGraw-Hill.
4. Fillmore, C. J. (1968). The case for case: Universals in linguistic theory. In E. Bach & R. T. Harms (Eds.), Universals in linguistic theory (pp. 1–88). Holt, Rinehart, and Winston.
5. Fillmore, C. J. (1969). Types of lexical information. In D. Reidel (Ed.), *Studies in syntax and semantics* (pp. 109–137). D. Reidel Publishing.
6. Fillmore, C. J. (1977). The case for case: Grammatical relations. In P. Cole & J. M. Sadock (Eds.), *Syntax and semantics* (Vol. 8, pp. 59–81). Academic Press.
7. Fillmore, C. J., & Atkins, B. (1998, May 28–30). FrameNet and lexographic relevance. Paper presented at the Granada Symposium on Lexography, Granada, Spain.
8. Jackendoff, R. (1977). *Constraints on grammar: Generative grammar and the syntax of English*. MIT Press.
9. Jerono, P. (2011). *Kishazi huru cha Kiswahili: Mtazamo wa X-bar* (Unpublished master's thesis). University of Nairobi, Nairobi, Kenya.
10. Kwambai, M. (2022). Amezidi Imezidi. *Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)*, Editon Consortium Publishing.
11. Mel'cuk, M. I. (1998). *Course in lexical semantics*. Bradford Books (an imprint of MIT Press).
12. Murage, J. N. (2011). *Uhakiki wa fani katika Utendi wa Mwana Ninga: Nadharia ya Umuundo* (Unpublished master's thesis). University of Nairobi, Nairobi, Kenya.
13. Talmy, L. (2000). The semantics of causation. In; *Toward a cognitive semantics* (pp. 123–143). MIT Press.
14. Talmy, L. (2000). *Toward a cognitive semantics*. MIT Press.
15. Tannen, D. (1987). *That's not what I meant!*. William Morrow Paperbacks.
16. TUKI. (1981). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford Publishers.


Copyright © 2024: by the author/s. This article is licensed and distributed under an Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International (CC BY-NC-SA 4.0)